**SIKILIZA UJIFUNZE KUHUSU AFYASEHEMU YA NANE**

KUHUSU MALARIA, KUTEMBELEA WAGONJWA HOSPITALI, VYANDARUA VYA KUZUIA MBU

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

## Utangulizi

Hujambo na karibu kwenye sehemu nyingine ya mchezo wa kuigiza kuhusu afya katika kipindi cha sikiliza ujifunze. Leo utawasikia Manuel, Simo, Steve Jimmy na Hassan wakiendelea na shughuli zao za kila siku huku wakiendelea kukabiliana dhidi ya maradhi. Wawili kati yao wanapaswa kwenda hospitali. Vijana hawa wanalazimika kukabilina na panda shuka za kimaisha peke zao kwa sababu wanaishi mjini bila ya wazazi wao kwa kuwa walikuja kutafuta masomo kutokana na kukosekana shule za upili kijijini mwao. Wanaishi katika bweni la Mandela na mwenye nyumba wao hawajali sana la zaidi analohitaji ni pesa zake tu za nyumba, kutokana na hilo mara nyingine maisha yanaweza kuwa magumu na hasa panapozuka maradhi mazito. Tega sikio basi usikie jinsi vijana hao wanavyojaribu kukabiliana na hali hiyo, na mwisho tutakupa maelezo kidogo juu ya kujiepusha na maambukizi kutokana na mbu wanaoeneza Malaria.

## Tukio la kwanza

*Jimmy, Manuel, na nesi wa kiume, katika kiliniki saa za asubuhi. Hakuna shughuli nyingi, watoto wanalia, wagonjwa wengine wanakohoa, kuchemua, na sauti mbali mbali zinasikika.*

*SFX* — *Mlango wafunguka. Sauti ya kiume yasikika - anaita:*

Nesi: Nani mwengine tafadhali?

Jimmy: Habari za asubuhi Sir. Jina naitwa Jimmy na huyu ni rafiki yangu Manuel, ninaumwa sana na sijui tatizo ni nini...

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

Nesi: Kwa jumla unajihisi vipi?

Jimmy: Nimepoteza hamu ya kula… natapika kila kitu nnachokula, tumbo linaniuma, nina maumivu ya viungo na homa isiyoondoka na dalili nyingine.

Nesi: Naam, kijana, dalili hizo ulizozitaja inaonesha umepata malaria. Nitakachofanya kwa sasa ni kukupima ikiwa kweli una malaria, halafu nitakupa matibabu. kwanza lete mkono...

*SFX* *Sauti ya kiti kinazogezwa, vifaa vya matibabu vinasikika vikigongana na mfuko wa plastiki unafunguliwa.*

Nesi: Tazama Jimmy, sindano hii ni mpya haijatumika...

Jimmy: Auchh…

Nesi: Ok sawa tumemaliza... sasa subiri dakika 30.

Manuel: Wapi? Hapa sio?

Nesi: Hapana subirini hapo nje... kuna viti vya kukaa…

*SFX* *Sauti za kutembea na wanakaa kwenye viti vya mbao kisa kinaendelea kliniki.*

Jimmy: Najisikia kizunguzungu Manuel… ngoja nijilaze hapa kwenye benchi...

Manuel: Njoo hapa Jimmy… lala hapa, nitegemee mimi...

Jimmy: Natumai nesi atamaanisha dakika 30 kweli...

Manuel: Hiyo itategemea ikiwa atatazama saa yake... mara nyingine wajua hizi saa huwa za mapambo tu...

Jimmy: Ni kweli... (anataka kutapika). Ahhh! nachukia hali hii... ya kujihisi kama nataka kutapika halafu sitapiki,,yaani unahisi kama utumbo wote umejisokota kwenye moyo na mbavuni ...lo!

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

*SFX* *Sauti ya mtu akija.*

Nesi: Jimmy na rafiki yako mnaweza kuja tafadhali... matokeo ya uchunguzi yako tayari.

*SFX* *Sauti ya viti na meza vikisogezwa.*

Nesi: Jimmy nimegundua viini vya malaria kwenye damu yako... ntakupa dawa.

Manuel: Dawa zote hizo nesi zitaingia kwenye Tumbo la Jimmy?

Nesi: Sio kwa mara moja lakini… mkifika nyumbani meza tembe nne mara moja... halafu tembe mbili ya kila dawa hizi kwa siku tatu zijazo. Usisahau kunywa maji mengi au maji ya matunda. Ni muhimu sana umalize dosi vinginevyo dawa hazitofanya kazi vizuri.

Jimmy: Kwa hivyo kimsingi baada ya kutumia hizi dawa ntajisikia vizuri na kurudi katika hali yangu ya kawaida niweze kwenda shule?

Nesi: Ndio. Lakini sifikiri kama una tatizo hilo moja tu. Ningekushauri uende ukapimwe zaidi. lakini itakugharimu pesa zaidi.

Manuel: Lo, nesi wataka kusema hivyo ulivyo mpima rafiki yangu ina maana sio uchunguzi wa kisawasawa? sasa hii kliniki ni ya nini hapa ikiwa hali ni kama hii?

Nesi: Sii tunatoa ushauri na kutibu maradhi madogo tu. kwa upande wa rafiki yako ana maradhi mazito. Homa yake ni kali mno. Na hali hii huenda imesababishwa na viini vya malaria. Au kidonda chake kimepata tetenus, sijui...

Manuel: Bado sijafahamu kwa nini muwe hapa... ushauri mnaotoa

unapatikana kwenye vitabu... tunaweza hata kujisomea sisi wenyewe...

Nesi: Ni kweli unayosema Manuel… Lakini maelezo ya hospitali hayamo kwenye hivyo vitabu... tunaelewana vijana?

Jimmy: Manuel twende zetu... nataka tu kwenda nyumbani...

Nesi: Pamoja na kwamba mnalalamika sana kwamba sijamtibu Jimmy vizuri. Ngoja niwaulize kitu kimoja, je mnalala kwenye chandarua cha kujikinga na mbu?

Jimmy: Mnatoa vya bure hapa?

Nesi: Hapana lakini ningependa kuwaambia kwamba ikiwa hamlalii chandarua kilichotibiwa ni bora muanze kulalia sasa hivi. Hii itasaidia kupunguza hatari ya kuambukizwa malaria... hii ni muhimu sana katika maisha yenu.

Manuel: Jimmy unacho chandarua lakini hukitumii...

Jimmy: Sina tena chandarua Manuel, Steve alikuza.

Nesi: Nunua kingine basi... hakina gharama yoyote...

Jimmy: Baadae sio sasa... Ntawezaje kununua kingine wakati siwezi kumudu hata matibabu.

Nesi: Kwanini msiulizie ikiwa mnaweza kupata vyandarua vya bure kutoka shirika lisilo la kiserikali liko hapo tu mlango wa pili? Wanashughulika sana na masuala ya msaada wa matibabu. Nyie bado ni wanafunzi… Nafikiri watawasaidia... mwajua kinga ni bora kuliko tiba. Lazima muweke usafi pia katika mazingira yenu mnayoishi. Halafu mtapunguza mbu... na hapo mtakuwa mmefanya jambo la maana la kuzuia kuambukizwa malaria... ni ushauri tu vijana, lakini kwa sasa nina wagonjwa wengine wa

kuwahudumia, kwa hiyo kwa herini vijana...

Manuel: Wagonjwa hao pia wako hapa kupata maagizo bora ya kiliniki?

Nesi: Sema unachotaka...

**Tukio la pili**

*Jimmy, Manuel, na Hassan katika bweni, asubuhi. Sauti ya mbu, vijana wakikoroma, mara moja moja wanajipiga makofi ya kuua mbu, na kukoroma kunatatizwa na sauti za mbu...*

Manuel: Wajisikiaje Jimmy? Dawa zinakusaidia?

Jimmy: (Kinyonge) Si hivyoo… Manuel naona hali yangu inazidi kuwa mbaya, naanza kuhisi vibaya hata nikimeza... hata sikuweza kumaliza kunywa juisi ulionipa.

Manuel: Pole sana, Jimmy.

Jimmy: (Kinyonge) Na hawa mbu washenzi hawataki kuniachia nafasi hata kigodo nilale...

Manuel: Hii sasa imezidi... ni kama hawa mbu wanyonya damu wameamua kufanya sherehe kwenye miili yetu....

*SFX* *Sauti ya mbu na kofi*

Manuel: Nimekupata... Shit! Cheki mbu huyu alivyoninyonya damu mwilini.

Hassan: Manuel nyamazeni! nataka kulala... tujaribu kujifunika na blanketi kuanzia miguu mpaka kichwa.

Jimmy: (Kwa sauti ya unyonge) Nimeshapata kisomo kuhusu nini maana ya malaria… siwezi hata kidogo washikaji kujihatarisha kuumwa

na mbu... hata kama kuna joto ntajifunika gubigubi ntavumilia joto....

Manuel: Siwezi kujizika mzima blanketini... ngoja nivae shati...

*SFX* *Sauti ya kitanda*

Manuel: Vipi washikaji silioni shati langu la mikono mirefu.....

Hassan: Inaonekana humo ndani kuna mtu anapia bei vitu vyetu...

Manuel: Inawezekana ni panya... wanaweza kufanya chochote mapanya ya humu ndani...

Jimmy: (Kwa unyonge) Acheni mchezo jamaa! panya anawezaje kuchukua fulana nzito kama ya Hassan?

Manuel: Acha utani hapa! namaanisha huyu panya ni panya mtu!

Hassan: Manuel haitachukua muda mrefu tutamkamata tu mwizi... siku za mwizi ni arobaini!

Manuel: Mwajua washikaji inaonekana vitu vyetu vingi vinatoweka na vyote kwa njia za hivi hivi tu..nafikiri tungeanzisha mfumo mpya wa kuwazuia hawawezi wa humu ndani...

Hassan: Kwanza tushughulikie hili la mbu... hayo mengine yatafuata kwa wakati wake.

Jimmy: (Kwa unyonge) Manuel lazima umwambie yule rafiki yako bwana... mwenye nyumba… afanye kitu hapa bwana kuhusu haya mazingira machafu...

Manuel: Huo ni mzaha wa ghali ya juu Jimmy… tutaanzaje kumfuata ikiwa hatujamlipa pesa zake za kodi ya nyumba?

Jimmy: (Kwa unyonge) Wasema kweli Manu… basi kwa nini tusifanye vile daktari alivyosema? Alitaja kitu kuhusu mashirika yasiyo ya kiserikali...

Manuel: Ni wazo zuri sana hilo Jimmy! Ntakwenda kesho nikitoka shule nikaulize kama wanaweza kutupa hivyo vyandarua vya bure sote... pamoja na kina Simo na Steve.

Hassan: Wanishangaza sana Manuel, unapowahusisha Simo na Steve katika mpango huu... wewe hujagundua kwamba watu hawa wamepotea kabisa? Wanaishi katika sayari nyingine kabisa tofauti na sisi...

Manuel: Ni kweli Hassan… Ni siku ya pili leo hawa jamaa wamepotea… hawaji hapa...

Jimmy: Ingekuwa wamenipa pesa zangu mimi ningeweza kwenda nyumbani. Sasa itakuwa wako wapi?

*Muziki*

**Je wajua… malaria**

*Wazungumzaji wawili*

**Ukweli kuhusu Malaria**

Malaria ni mojawapo ya maradhi yanayoua watu wengi barani Afrika zaidi ya watu millioni moja wanakufa kutokana na malaria kila mwaka duniani.asilimia 90 wanakufa barani Africa.Japo kuwa maradhi haya yanawapata watu wa umri mbali mbali,zaidi unaua watoto na kina mama wajawazito.Unaambukiza watu kupitia mbu walio na viini vya Malaria wanapokuuma.

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

## Dalili

Madhara ya kwanza ya Malaria yanaonekana kwa kawaida baada ya siku 10 hadi 15.Dalili hizi ni pamoja na homa,kichwa kuuma,kutapika na kuhisi baridi.Ikiwa hutatibiwa haraka unaweza kuzidiwa na hata kufariki.

## Tiba

Ukihisi kwamba huenda ukawa unaugua malaria,hakikisha kwamba sio tu ni homa ya kawaida kabla ya kumeza dawa yoyote.Kuhakikisha nenda ukapime damu.Malaria unatibika ukigunduliwa mapema.Kwa hivyo lazima ufanyiwe uchunguzi haraka iwezekanavyo.Kuna dawa mbali mbali za kutibu malaria madukani lakini ni muhimu kuwa muangalifu kwa sababu sio dawa zote ni nzuri. Pata ushauri wa daktari ikiwezekana.

## Kinga

Njia nzuri ya kuzuia Malaria ugonjwa unaoua ni kujiepusha na kuumwa na mbu. Mbu huwa wengi zaidi nyakati za magharibi na usiku,kwahivyo unatakiwa kuvaa nguo za mikono mirefu na kulala ndani ya chandarua cha mbu. Chandarua kilichotibiwa na dawa ya kufukuza mbu. Dawa za kupuliza za kupambana na mbu zinaweza pia kusaidia. Hata hivyo usipulize dawa nyingi kupita kiasi mara nyingine zinakuwa na chemikali hatari za sumu. Wanawake wajawazito ndio walio hatarini zaidi kupata Malaria.

## Mwisho

Asante sana kwa kutegea sikio kipindi hiki cha sikiliza ujifunze juu ya afya. Mchezo huu umeandikwa na Hope Azeda na kuhaririwa na Saumu Mwasimba. Kumbuka unaweza kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaambia marafiki wasikilze kupitia njia ya Internet,anuani yetu ni www.dw-world.de mkwaju kiswahili. Hadi wakati mwingine kwa heri...